BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Nne – Tarehe 14 Septemba, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uvuvi, Nam. 7 ya 2010 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari kwa ajili ya Kusimamia, Kuendeleza Uvuvi na Kuhifadhi Maliasili za Bahari na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Uwekezaji:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi na Uwekezaji Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uvuvi, Nam. 7 ya 2010 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari kwa ajili ya Kusimamia, Kuendeleza Uvuvi na Kuhifadhi Maliasili za Bahari na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

60. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Mashindano ya Michezo ya Mabunge (Inter Parliamentary Games), ni nyenzo muhimu sana ya kuimarisha Diplomasia ya Mabunge na kutangaza utamaduni na utalii wa taifa.

(a) Kwa kushirikiana na Muhimili huu wa Baraza la Wawakilishi, je, Serikali ina mkakati gani wa kuziendea fursa hizo kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

(b) Ni lini Serikali kwa kushirikiana na Mihimili ya Baraza la Wawakilishi na Mahkama, itaanzisha mashindano maalum yatakayokuwa na lengo hilo la kuimarisha Diplomasia ya Mabunge na kutangaza utamaduni na utalii wa taifa.

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

218. MHESHIMIWA MOHAMMED MANZI HAJI (Jimbo la Mwanakerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kwa kuwa mafanikio ya matibabu na urekebishaji wa waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya yanategemea pia ufuatiliaji na urejeshwaji wao katika jamii.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa ufuatiliaji baada ya matibabu ya waathirika hao.

(b) Ni watu wangapi wanaendelea kufuatiliwa baada ya kurejea katika jamii.

(c) Je, ni waathirika wangapi walirudia matumizi ya dawa za kulevya baada ya kurejea katika jamii.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

263. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

(a) Ni lini Serikali itaanza kulipa stahiki na maslahi ya Waheshimiwa Madiwani kwa kiwango kitakachofanana na hadhi yao kama Wawakilishi wa Wananchi wa kuchaguliwa kwa kura.

(b) Ni lini Serikali itampatia usafiri wa gari Mwenyekiti wa Baraza la Mji Mkoani Pemba, ili aweze kuyafikia maeneo yake ya utendaji bila ya usumbufu wowote.

## Wizara ya Fedha na Mipango:

48. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Zanzibar ina wafanyabiashara wengi wadogo wadogo na wa kati ambao hufanya shughuli zao katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kadhaa kuhusiana na kodi nyingi na kubwa zinazowakabili.

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha Mfumo wa Kodi ili kuwasaidia wafanyabiashara hawa kukuza biashara zao.

247. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kuna utaratibu gani unaotumika wa kulipa pencheni za wastaafu pindi wakimaliza muda wao wa kufanya kazi.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

147. MHESHIMIWA MARYAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kazi kubwa ya usambazaji wa miundombinu ya maji katika kisima cha Ulenge. Hata hivyo, bado kuna kilio sugu cha upatikanaji wa maji katika maeneo ya Mkanyageni, Michenzani, Kisiwapanza, Shidi na maeneo mengine ya jirani ndani ya Jimbo la Mkoani.

Ni lini Serikali itakamilisha uunganishaji wa miundombinu ya maji kutoka katika kisima cha Ulenge kwenda maeneo ya Michenzani na Mkanyageni, ili kuwapatia wananchi wa maeneo hayo haki yao ya msingi ya kupata maji safi na salama.

307. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Utaratibu wa kupata tokeni za umeme unakuja baada ya kulipia na kutambulika kwa mita husika.

(a) Ni lini utaratibu uliopo wa mteja kwenda kuingiza tokeni kwenye mita utaondoka na tokeni zikaingia *automatically*.

(b) Kwa kiasi gani wateja wetu tunawasumbua kwa kuwa na utaratibu uliopitwa na wakati.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

121. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Imebainika kuwa ni takriban miezi michache iliyopita kumekuwa na ongezeko kubwa la bei za bidhaa mbalimbali hapa Zanzibar.

(a) Je, sababu zipi zilizopelekea bei za bidhaa kupanda maradufu na kuchochea maisha ya wananchi kuwa magumu.

(b) Serikali ina mpango gani wa kuendelea kufidia gharama za bidhaa ili kupata unafuu wa matumizi kwa dhamira ya kuwahurumia wananchi wake.

(c) Je, wananchi wa Zanzibar watarajie lini kuwa wataepukana na hali hii ya ugumu wa maisha.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

1. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Zanzibar ni moja kati ya nchi zilizobarikiwa sana katika historia na mambo ya kale kutoka karne ya 15, hali inayoifanya kuwa moja ya nchi yenye vivutio vikubwa vya watalii kuja nchini, mfano ukitolewa kwa Magofu ya Mkama Ndume yaliyopo Pujini kisiwani Pemba.

(a) Je, Serikali imechukua jitihada gani kuyaendeleza Magofu ya Mkama Ndume yaliyopo Pujini, ili kuzidi kuwavutia watalii.

(b) Kwa kuwa bustani ya Forodhani ni moja wapo mwa kivutio kikubwa cha utalii hapa Zanzibar, je Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vijana wa Makachu kufanya shughuli zao kwa utulivu na usalama wa afya zao.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

107. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi

Wafanyabiashara wa mihogo na ndizi kutoka Pemba kuja Unguja, wamejikuta kwenye wakati mgumu sana wakiwa bandarini kwa kutakiwa kulipa ushuru (*wharfage*) na wanapofika na mzigo wao Unguja.

Je, Serikali ina msaada gani wa kuwaondolea ushuru wafanyabiashara ya mihogo na ndizi ambao wanasafirisha bidhaa hizo kwa Unguja na Pemba.

144. MHESHIMIWA AZA JANUARY JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Mfumo wa sasa wa usajili wa namba kwa vyombo vya moto vyenye maringi mawili hadi matatu unaanza na herufi **M** na vyombo vyenye maringi manne unaanza na herufi **Z.**

(a) Nini maana ya hizi herufi ambazo zinatumika katika usajili wa vyombo hivi.

(b) Ni kitu gani kilichosababisha herufi hizi zisiongezeke katika zile herufi za zamani.

293. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Mabasi ya Umeme yameanzishwa ili kuboresha usafiri wa umma, lakini gharama za usafiri zinaweza kuwa mzigo kwa wanafunzi na walimu wanaosafiri kila siku kwa kutumia mabasi hayo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka nauli maalum yenye punguzo kwa wanafunzi na walimu wanaotumia Mabasi ya Umeme.

(b) Ni utaratibu gani utakaotumika kuwatambua wanafunzi na walimu wanaostahiki kupata punguzo hilo.

(c) Kwanini Serikali haioni haja ya kuanzisha tiketi maalum za wiki au mwezi kwa wanafunzi na walimu, ili kupunguza gharama zao za usafiri.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

90. MHESHIMIWA SAID ALI JUMA (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Nchi yetu ina mahitaji makubwa ya nguvu kazi ya Kitaifa ya vijana lakini tunashuhudia vijana wengi hawajajikita katika Sekta ya Kilimo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashajihisha na kuwawezesha vijana waweze kushiriki katika Sekta ya Kilimo.

**<u>Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:</u>**

129. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Suala la michezo sio jambo la Muungano na ndio maana Tanganyika na Zanzibar kila moja ina ligi kuu yake. Kutokana na hali hiyo Zanzibar inapigania uanachama katika Shirikisho la Mpira wa Miguu Barani Afrika “CAF”. Ni muda mrefu sasa tumeshuhudia na kuona michezo mbalimbali ya mpira wa miguu ya Ligi ya Tanganyika zikichezwa katika Viwanja vya Zanzibar.

(a) Je, ni utaratibu gani na sheria ipi inayotumika hadi kupelekea ligi ya Tanzania Bara kuchezwa Zanzibar hali ya kuwa michezo sio suala la Muungano.

(b) Kwa kuwa wakati wa bajeti Serikali ilitueleza kwamba wameanza kuchukua hatua za kurejesha uanachama wa Zanzibar katika CAF. Je, harakati hizi zimefikia hatua gani.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

231. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali imeifuta kampuni ya ZAFICO, licha ya kazi mbalimbali zilizokuwa zikifanywa na kampuni hiyo.

Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea kufutwa kwa Kampuni hiyo ya Uvuvi.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uvuvi, Nam. 7 ya 2010 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari kwa ajili ya Kusimamia, Kuendeleza Uvuvi na Kuhifadhi Maliasili za Bahari na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**14 Septemba, 2026.**

**(Ramadhan Khamis Juma)**
**KAIMU KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**